

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

Simu: +255-26-2323201-7
Nukushi: +255-26-2323208
Barua pepe: nje@nje.go.tz
Tovuti: www.foreign.go.tz



Mji wa Serikali,
Mtumba,
S.L.P 2933,
40466 DODOMA

TAARIFA KUHUSU WATANZANIA NCHINI UKRAINE.

Dar es Salaam, 09 Machi 2022

Kundi la mwisho la wanafunzi 32 waliokuwa wamekwama katika mji wa Sumy limeondoka kwa mabasi kuelekea katika miji ya Poltavo na Lviv nchini Ukraine na kisha kuingia katika nchi za Hungary na Poland.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya mazungumzo yaliyofanyika kwa njia ya simu kati ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Ukraine Mhe. Dmytro Kuleba tarehe 07 Machi, 2022, kwa lengo la kuiomba Serikali ya Ukraine kusaidia kuwatoa Watanzania wanaosoma katika chuo cha Sumy.

Katika Mazungumzo hayo, Naibu Waziri Kuleba aliridhia ombi la kuwasaidia wanafunzi hao kuondoka nchini Ukraine salama kupitia mipaka ya Poland na Hungary kwa utaratibu ulioratibiwa na Balozi za Tanzania nchini Sweden, Ujeruman pamoja na Urusi na kusimamiwa na uongozi wa chuo cha Sumy.

Aidha, wanafunzi wengine 61 waliondoka katika chuo cha Sumy alfajiri ya Machi 08, 2022 ambapo 50 kati yao wanatarajiwa kuingia nchini Hungary na 11 nchini Poland. Maafisa wa Balozi za Tanzania nchini Sweden na Ujerumani wako tayari kwenye mipaka ya Poland na Hungary kwa ajili ya kuwapokea wanafunzi hao pindi watakapowasili mpakani.

Kadhalika, wanafunzi 11 waliotoka kwenye Chuo Sumy kupitia njia salama 'Safe Corridor' iliyotolewa na Serikali ya Urusi, wamefanikiwa kuingia nchini Urusi na tayari wamepokelewa na Ubalozi wa Tanzania uliopo Moscow Urusi.

Balozi za Tanzania nchini Sweden na Ujerumani zimetoa namba maalum kuwawezesha wanafunzi hao kuwasiliana na Maafisa wa Balozi hizo pindi wanapowasili mipakani ambapo kwa mpaka wa Poland namba za simu (+46720494576) na kwa mpaka wa Hungary namba za simu (+4915215117558).

Kwa hatua hiyo, tunapenda kuwaarifu Watanzania wote kuwa hivi sasa hakuna mwanafunzi kutoka Tanzania aliyebaki kwenye Chuo cha Taifa cha Sumy kilichopo nchini Ukraine.

Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inawashukuru kwa dhati Watanzania (Diaspora) wanaoishi Ukraine, Poland, Romania na Hungary, pia Mkurugenzi wa Global Education Link, Bw. Abdulmalik Mollel na Kamati ya Wazazi wa wanafunzi kwa utulivu wao na kuisaidia Serikali kutekeleza wajibu wake bila shinikizo na kufanikiwa kuwaondoa Watanzania wote nchini Ukraine wakiwa salama.

Mwisho Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inawashukuru wote walioshirikiana na Serikali kuwezesha kuwaondoa salama wanafunzi hao. Pia tunawashukuru Watanzania na wazazi wa wanafunzi kwa uvumilivu na uelewa wao iliowezesha Serikali kutekeleza wajibu wake.



Emmanuel Buhohela

Mkurugenzi wa mawasiliano Serikalini